

FOMU YA MKATABA WA UJENZI

A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA

1	MWAJIRI	Mkuu wa Chuo VETA Dodoma S. L. P. 2197, Dodoma - Tanzania
2	JINA NA ANWANI YA FUNDI (Mwajiriwa)	Jina: ... EXAVERY A. Ngowi, Anwani: ... CHEMBA ... Simu: Account number.....
3	ENEO LA UJENZI	CHEMBA -DVTC
4	MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI	KUFANPAZA MFUMO WA MASHARTI (MAREHITO 15)
5	GHARAMA YA UFUNDI	4,500,000/=
6	MUDA WA MKATABA (Tangu Kusainiwa kwa Mkataba):	Tarehe ya Kusaini Muda: 20 ... (Siku) Tarehe ya Kuanza Kazi 09/02/2022. Tarehe ya Kumaliza Kazi 01/03/2022
7	MASHARTI YA MALIPO:	<ul style="list-style-type: none"> • Hakuna Malipo ya Awali • Fundi atalipwa kwa awamu baada ya kazi husika kukamilika na kukaguliwa

B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

1. Mwajiri atatoa vifaa vyote vya ujenzi kulingana na maelekezo ya *Mtaalamu Mshauri*. Zaidi ya hayo mwajiri atatoa maji na umeme.
2. Mwajiri atatoa vitendea kazi vyote kama "concrete mixer", toroli, karai, ndoo, chepe, ngazi, n.k.
3. Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa mchanganuo wa kazi na mwongozo wa *Mtaalamu Mshauri*, kwa umakini na uhodari wa hali ya juu wa kiufundi.
4. Fundi asipofanya kazi yake vizuri, Mwajiri ana haki ya kumsimamisha kazi na kulipa hasara zote zilitokana na uzembe au makusudi.
5. Fundi atatoa maelekezo ya kazi kwa vibarua wake na atahusika moja kwa moja kwenye ujenzi kwa kutumia vibarua wake na kuwaunganisha mafundi wote aliowaajiri kuhakikisha kazi inafanywa kulingana na taratibu za kiujenzi.
6. Fundi kwa wakati wote anatakiwa kuhakikisha yeye pamoja na mafundi wake wanazingatia nidhamu na tabia njema na asiajiri kabisa mtu asiyekuwa na utaalumu au ujuzi wa kutosha.
7. Fundi atahusika na vitendo (*kama wizi, uharibifu wa mali za chuo*) vyote vinavyofanywa na mafundi wake na mtu yeyote anayefanya kazi chini ya usimamizi wake.
8. Fundi kwa wakati wote ahakikishe kuwa eneo la kazi linakuwa safi na salama na pia pindi kazi iishapo ahakikishe vifaa vyote vilivyosalia katika eneo la ujenzi kama mabaki vimewekwa sehemu husika na kuacha eneo likiwa safi na salama.
9. Kiasi cha asilimia 5% ya kiasi cha mkataba kitashikiliwa na Mwajiri kwa muda wa Miezi Mitatu baada ya kazi kukamilika (*Retention Money*) na kulipwa mara baada ya ukaguzi wa mwisho kufanyika.
10. Ucheleweshaji wa Kazi:
 - Ucheleweshaji wa kazi uliosababishwa na fundi, fundi atapewa adhabu ya kulipa kiasi sawa na hasara iliotokana na ucheleweshwaji huo.

11. Ucheleweshaji wa Vifaa na Malipo:

- Ucheleweshaji uliosababishwa na Mwajiri (*kutokana na fedha au vifaa*), Fundi ataongezewa muda wa kumaliza kazi.

12. Uvunjwaji wa Mkataba:

- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Mafundi walioko chini yake au vibarua wake watajihusisha na wizi wa vifaa vya ujenzi au mali yoyote ya Chuo.
- Mkataba utavunjwa iwapo; Fundi au Fundi wake hatazingatia taratibu za ujenzi au ubora wa kiufundi katika kazi yake, ikiwemo kufuata michoro au maelekezo ya Mtaalamu Mshauri.

MWAJIRI:

Saini:

Jina:

Cheo:

Tarehe:

FUNDI/KIBARUA

Saini:

Jina:

Cheo:

Tarehe:

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini:

Jina:

Cheo:

Tarehe:

SHAHIDI WA FUNDI/KIBARUA

Saini:

Jina:

Cheo:

Tarehe: